


Mazungumzo ya Justin na Mage kuhusu taa za mwanga wa jua





Habari, Mage Hujambo?

Nzuri, na wewe?



Sijambo. Umeishaona taa yangu mpya ya mwanga wa jua?

Hapana. Ikoje?



Ni ya ajabu! Ninaweka paneli ya sola juu ya bati na inatoa umeme nyumbani kwangu.

Inafanyaje kazi?



Ndani ya paneli kuna seli maalum zitoazo mwanga zikipata mionzi ya jua.

Lakini si hakuna jua wakati wa usiku!



Ndiyo maana nina betri. Mchana umeme unaenda katika betri na kuhifadhiwa hadi usiku ambapo taa huwaka kwa umeme kutoka kwenye betri.



Naweza kutumia betri ya gari?

Ndiyo, lakini betri za sola ni bora zaidi na zinadumu zaidi.

Kwa sasa huhitaji tena kununua mafuta ya taa?

Ni kweli. Na tunatunza pesa sasa.



Taa za sola zina mwanga kuliko taa za mafuta ya taa. Watoto wetu wanaweza kusoma wakati wa usiku.



Hilo ni la muhimu zaidi.

Na taa za mwanga wa jua hazina moshi ndani kama taa za mafuta.

Najua hilo na ni nafuu kwa afya ya familia yako yote!



Na taa ngapi unaweza kuziwasha kwa paneli moja?

Hii hutegemea ukubwa wa paneli na aina ya taa unazotumia.



Baadhi ya paneli ni kubwa sana na baadhi ni ndogo kuweza kutosha ndani ya mfuko wa nguo yako.



Hivyo nikipata paneli kubwa itafua umeme zaidi na kuwasha taa nyingi?


Ni kweli!





Ni aina gani ya taa unazozielezea?

Ni zenye ukungu, zaweza kuwa tube ndefu au zilizopinda pinda kama zile za kawaida zinazojulikana kama kutumia umeme kidogo.



Nimekwisha zitambua hizo na za LED ni zipi?

LED huwakilisha "Light Emmiting Diode"; diode ni kifaa cha electroniki kinachotoa mwanga.



Hivyo zipi ni nafuu?

Taa za ukungu ni nafuu lakini zinatumia nishati zaidi ya zile za LED.



Nikitumia za LED nitakuwa na taa nyingi zaidi katika mfumo wangu wa sola.

Ni kweli!



Lakini uwe makini. Kuna taa za LED bora na zina mwanga mkali na zinadumu sana na zingine zina ubora mdogo na ni nafuu pia.

Nitatafuta kampuni ninayoiamini ili iniuzie bidhaa za sola.



Ni hivyo tu ninavyohitaji: paneli za sola, betri na taa ya sola?

Kuna kitu kimoja. Bado unahitaji kidhbiti betri, kifaa hiki kinalinda berti ili idumu kwa muda mrefu zaidi.

Kinafanyaje kazi?

Kinazuia betri isizidiwe chaji wala kupungukiwa chaji chini ya kiwango.



Njia rahisi ni kununua mfumo kamili ili kuweza kujua kwamba kila kitu kipo pamoja na kwenda kufungiwa mfumo wako.



Sasa nimeelewa zaidi juu ya mfumo wa taa za mwanga wa jua. Ila sijui ni paneli zipi au taa za sola zipi ninazoweza kununua.




Unaweza kupata kifurushi cha taa za LED kama zile za TanzSolar. Taa hizi zina betri na paneli na kidhbiti betri.



Ndiyo, nazijua na taa hizo zinafanya kazi vizuri na zinawaka sana.

Au unaweza kupata kifurushi cha paneli kubwa, betri, kidhbiti betri, inveta na waya. Ambapo ukielekezwa utafunga wewe.



Ni vizuri kuwa na taa nyingi katika mfumo. Ni kipi kingine ninachoweza kukitumia kwa umeme wa sola?



Unaweza pia kuchaji simu, kuwasha radio, TV, dish hata friji maalum au ya wastani. Lakini utahitaji mfumo mkubwa ili kuzalisha nishati ya kutosheleza TV au friji.

Baadhi ya vitu hutumia umeme zaidi ili kuwaka, mfano majiko, friji na pasi za umeme.

Labda uwe ni mfanya biashara au taasisi ya serikali, vituo vya afya mashule na kliniki, sehemu hizi huhitaji mifumo mikubwa zaidi kuwasha vifaa mbali mbali.

Nafikiri nitaanza na mfumo wa kawaida kwa ajili ya taa na kuchaji simu.

Ndivyo nilivyofanya nami nafurahi kuwa na taa nyumbani na kuweza kutunza pesa bila kununua tena mafuta ya taa.

Ndiyo, familia yangu pia itafurahia. Wanangu watafanya vizuri shuleni kama watasoma usiku na sote tutakuwa wenye afya njema bila moshi utokanao na kuungua kwa mafuta ya taa.

Asante sana kwa kunielewisha juu ya mfumo wa umeme wa sola.

Asante, natumaini unafurahia taa zako mpya za mwanga wa jua.

TANZSOLAR

A nonprofit company dedicated to bringing clean energy to rural villagers of Tanzania.



TanzSolar is:

- ☀ Bringing you **QUALITY PRODUCTS**
- ☀ Helping you **SAVE MONEY** by avoiding kerosene purchases
- ☀ Sharing **INFORMATION** about solar electricity.
- ☀ Keeping you in **GOOD HEALTH** with clean air to breathe.
- ☀ Assisting your children's education with **BRIGHT LIGHTS** to read by.
- ☀ Providing **REPAIRS** and **SERVICE** to keep your solar equipment working.
- ☀ Offering **LOW PRICES** with no profits to the company.
- ☀ Conveniently located in **MUSOMA**.
- ☀ **REACHING OUT** to you at your local markets.



Published with assistance from the Tanzania Rural Energy Agency



TanzSolar Ltd.



TANZSOLAR LTD.
6Q MAJITA ROAD MUSOMA 0652 094 421
WWW.TANZSOLAR.COM